

Sera: Sera ya Usaidizi wa Kifedha

Lengo:

Lengo la sera hii ni kutoa miongozo kwa ajili ya; WAGONJWA AMBAO HAWAJAFIDIWA KABISA NA WALIOFIDIWA ILA KWA KIWANGO CHA CHINI ikiwa ni pamoja huduma muhimu za dharura na nyinginezo.

Ufafanuzi:

FPL: Kiwango cha Umaskini cha Shirikisho (Federal Poverty Limit)

Kiwango cha chini cha bima- kiwango cha bima kinachoshughulikia matibabu

Kutokuwa na bima - watu ambao hawana bima

Mapato ya Familia - mapato ya jumla ya familia kwa nyumba

Usaidizi wa Kifedha: wakati ambapo mgonjwa ameidhinishwa ili kupokea Uhisani kulingana na kutokuwa na uwezo wa kulipa.

Mchango kwa ajili ya Huduma - Punguzo lililotolewa na U of U Health linalolenga kupunguza mzigo wa kifedha kwa wale wagonjwa wasiokuwa na bima.

AGB - Kiwango cha Kimsingi cha Fedha Kinachoandaliwa Bili (Amounts Generally Billed).

Iliyokotolewa kwa kugawanya Kiwango cha Jumla cha Bima Kinachoruhusiwa

kikigawanywa na Matozo yaliyotumwa kwenye bili ya bima, kwa kutumia mbinu ya kuangalia miezi 12 iliyopita.

Upeo:

Hakikisha kwamba Chuo Kikuu cha University of Utah Health, kinachofahamika hapa

kama U of U Health kinatimiza kikamilifu azimio lake pamoja na kujitolea kwa

wagonjwa/wadhamini wasiokuwa na ufadhili au waliofadhiliwa kwa kiwango kidogo

sana kwa hali inayoendelea. Usaidizi wa kifedha hutolewa kwa wale

wagonjwa/wadhamini wasioweza kutimiza wajibu wao wa kifedha. Uhitaji wa

kimatibabu na sera za ukubalifu wa kifedha wa idara kjutumika. Matozo ambayo

hayashughulikiwi pamoja na yale yasiyoruhusiwa yanaweza kukubalika kwa usaidizi wa

kifedha kwa madai ya huduma kwa Medicaid na programu za huduma za Indigent.

Maelezo:

- A. Usaidizi wa Kifedha unaelezewa kama huduma ambayo wagonjwa /wadhamini hudhirisha hali ya kutokuwa na uwezo wa kulipia huduma zinazotolewa ama

wanaweza kulipia sehemu ndogo ya ada ya huduma zinazotolewa. Malipo yoyote yanayolipwa kabla ya kutuma maombi ya Usaidizi wa Kifedha hayatajumuishwa kwa sababu uwezo wake wa kulipa tayari umeshabainishwa hapo awali. U of U Health hutumia kipimo cha kiuchumi ili kutoa usaidizi kulingana na mapato ya FPL* ambayo hayatazidi 300% ya mapato hayo ya FPL ili kuamua iwapo usaidizi huo utakuwa wa kiwango kidogo ama usaidizi kamilifu (soma jedwali hapo chini).

FPL %	Assistance Discount
≤ 150%	Full Charity (100%)
151% to 200%	99% - 67%
201% to 250%	67% - 33%
251% to 299%	33% - 1%

Uidhinishaji wa usaidizi wa kifedha huzingatia uthibitishaji wa mapato ya familia nyumbani, ukubwa wa familia nyumbani na kuanzisha utaratibu unaofaa. Ukumbwa wa familia nyumbani hutegemea pakubwa miongozo ifuatayo iliyo sawa na ile miongozo ya IRS kwa ajili ya kuamua wategemezi.

1. U of U Health inaweza kuhitaji nyaraka zifuatazo ili kuamua ustahiki wa usaidizi wa kifedha:
 - i. Fomu ya kifedha iliyojazwa kikamilifu
 - ii. Barua inayoelezea hali halisi ya sasa ya kifedha
 - iii. Nakala ya taarifa ya (za) sasa ya benki
 - iv. Nakala ya matokeo ya ushuru ya mwaka uliotangulia
 - v. Nakala ya kipande cha karatasi ya hundi kinachosalia kwenye kitabu na/ ama mapato mengine kutoka kwa miezi miwili (2) iliyopita
- B. U of U Health inaelewa kwamba baadhi ya wagonjwa wanaweza kushindwa kujaza kikamilifu fomu ya usaidizi wa kifedha, kuyafikia maagizo ya ukusanyaji wa nyaraka hizo, ama kwa vinginevyo wasijibu kwa kufuatia utaratibu huo wa kutuma maombi. Matokeo yake, pawaweza kuwa na hali ambazo ufaulu wa mgonjwa huyo wa kupata usaidizi wa kifedha huanzishwa bila ya kukamilisha usaidizi rasmi wa ombi. Katika hali hizi, U of U Health inaweza kutumia mbinu nyinginezo za kupata taarifa ili kufanya utathmini wa kibinafsi wa mahitaji ya kifedha. Kadhalika, ofisi ya ripoti za mikopo inaweza kutumiwa ili kufanya maamuzi ya ustahiki. Taarifa itaiwezesha U of U Health kufanya maamuzi ya kihakika kuhusu usaidizi wa kifedha wa wagonjwa ambao hawakuweza kujaza fomu ya maombi kwa kutumia makadirio bora yanayopatikana kutokana na ukosefu wa taarifa iliyotolewa moja kwa moja na mgonjwa.

- C. Ikiwa taarifa inayohitajika haikupokelewa, iliyobaki itakuwa ni jukumu la mgonjwa/mdhamini kama ilivyoratibiwa kwenye Sera ya Makusanyo ya Kujilipia ya Chuo Kikuu cha Utah Health.
- D. Gharama ya huduma ya afya ya wale wasilipiwa fidia inayotolewa kwa indigent itapangiwa, kuwekewa bajeti na kuripotiwa kwenye taarifa za kifedha za ndani na za nje za Hospitali ya U of U Health pamoja na UUMG kuambatana na kanuni za jumla zinazokubalika za uhasibu. Ujumla wa Kiasi cha Fedha Kilicholipishwa (AGB) kwa matozo ya mgonjwa kwa kwenda hospitali huamuliwa na mbinu ya Kisengerenyuma - Kituo cha sasa cha AGB cha Chuo Kikuu cha Utah ni 47%. Kufuatia maamuzi ya ustahiki kiwango cha pesa kilicholipishwa hakiwezi kuwa kikubwa zaidi ya Jumla ya Kiwango cha Fedha Kilicholipishwa.
- E. Mkurugenzi wa Fedha wa Hospitali ama Mkurugenzi wa Matibabu ana mamlaka ya kuidhinisha ama kukataa usaidizi wa kifedha ambayo hautimizi kigezo kinachohitajika.
- F. Vipindi vya Usaidizi wa Kifedha havitazidi muda wa miezi sita. Ikiwa pametolewa ombi la usaidizi linaloendelea ndani ya kipindi cha miezi sita, mgonjwa/mdhamini atalazimika kutuma upya ombi na kufikia viwango vya ufaulu vinavyohitaji baada ya kila miezi sita. Hospitali haitakubali maombi ya hapo awali ya kifedha katika utathmini wake unaofuata.
- G. Nakala ya Ombi la Usaidizi wa Kifedha, Maandalizi ya Bili ya Mtu Kujilipia, pamoja na Sera ya Ukusanyaji ama muhtasari wa lugha sahili wa sera hii unaweza kupatikana kwenye anwani zifuatazo:
1. Piga simu kwa (801) 587-6303
 2. Wavuti <http://healthcare.utah.edu/bill/#hardship>
 3. Ofisi ya Ushauri Nasaha wa Kifedha
 4. Ofisi ya Jengo la Huduma za Kibiashara
 5. Ni lazima maombi hayo yatumwe kwa barua ya posta kwenye PO Box 841482, Los Angeles, CA 90084-1482, kipepesi kwa (801)213-3385 au kwa kutuma baruapepe billing@healthcare.utah.edu
- H. Huduma zisizostahiki kupata usaidizi wa kifedha:
1. Huduma za pesa taslimu
 2. Huduma ya tiba ya meno zisizo za dharura
 3. Utumizi mbaya wa rasilimali za hospitali
 4. Utumizi mbaya wa huduma za dawa
 5. Kukataa kutuma ombi ama kufuatilia usaidizi uliopo
 6. Huduma zinazotolewa katika Kliniki ya South Main

KUTOBAGUA. U of U Health hakitengi, kunyima haki kwa, ama vinginevyo kubagua dhidi ya mtu yeyote kutokana na mbari, rangi, asili ya kitaifa, dini, jinsia, mwelekeo wa kijinsia, utambulisho/hali ya kujieleza kijinsia, taaarifa ya maumbile, hali ya kiuzoefu iliyolindwa, ama kutokana na ulemavu au umri katika kuingizwa kwa, ama kushiriki katika, au upokezi wa huduma na manufaa chini ya programu zake zozote na shughuli, ima iwe imetekelezwa moja kwa moja na U of U Health au kupitia kwa mkandarasi au wakala. Kwa taarifa zaidi kuhusu sera hii, wasiliana na ADA ya Chuo Kikuu/Mratibu wa Kitengo cha 504 katika: Mkurugenzi, Ofisi ya Nafasi Sawa na Hatua za Uthibitishaji, (801) 581-8365 (Voice/TTY), (801) 585-5746 (Kipepesi), au kupitia kwa Relay Utah kupitia kwa 711 au simu isiyolipiwa: (800) 735-2258 ama Spanish Relay Utah kupitia kwa: (888) 346-3162 .